
TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# Jarida

TOLEO No. 14 | Juni, 2025




# TMDA Yasaini Makubaliano ya Ushirikiano na Mamlaka ya Udhibiti ya Msumbiji



## Mafanikio Makubwa Uwekezaji viwanda vya Dawa: Uongozi wa TMDA Watembelea Viwanda vya Ndani

## Miaka Minne ya Uongozi wa Rais Samia:TMDA yajivunia mafanikio

# YALIYOMO


05 TMDA Yasaini Makubaliano ya Ushirikiano na Mamlaka ya Udhibiti ya Msumbiji

*Mnamo Tarehe 7 Mei 2025, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dr. Adam Fimbo na Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania, Bw. Pedro Davane kwa niaba ya Serikali ya Msumbiji, walisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika eneo la udhibiti wa dawa kati ya mamlaka za udhibiti wa nchi hizi mbili...*

**07 Naibu Waziri Aitaka MAB Kuboresha Upatikanaji wa Dawa Bora na Nafuu**

*Katika juhudi za kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania, Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mb), alikutana na Bodi ya Ushauri ya Wizara (MAB) tarehe 21 Februari, 2025, jijini Arusha.....*

10 Bidhaa Bandia Zakamatwa huku TMDA ikiimarisha Juhudi za Kulinda Afya ya jamii

*TMDA kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usimamizi wa sheria, imeimarisha nguvu katika kudhibiti usambazaji wa dawa bandia na zisizokidhi viwango kupitia operesheni maalum ya ukaguzi iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 8 Novemba, 2024....*

**12 Wizara ya Afya Yaunda Kikosi Kazi cha Uteketezaji Salama wa Vifaa Tiba Visivyotumika**

*Ili kukabiliana na ongezeko la vifaa tiba visivyotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara ya Afya imeunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kuratibu na kurahisisha uteketezaji wa vifaa tiba ambavyo havifai kwa matumizi...*

24 Mfumo wa Uteketezaji wa Dawa zisizofaa waimarishwa

*Ofisi ya TMDA Kanda ya Mashariki imeongeza juhudi katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa ujumla kwa kuhakikisha uteketezaji sahihi wa dawa na vifaa tiba vilivyopitwa na muda, bandia au visivyofaa kwa matumizi ya binadamu....*

# Karibu katika jarida letu Toleo la 14!

*Mpendwa msomaji,*



*Napenda tena kukukaribisha katika toleo letu la 14 la Jarida hili. Takribani mwaka mmoja umepita tangu tulipochapisha toleo letu la mwisho, na mafanikio mengi yamepatikana ambayo yanastahili kuripotiwa.*

*Ndani ya TMDA, tunashuhudia maendeleo makubwa katika mifumo iliyopo ya kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi. Mifumo yetu ya udhibiti imetathminiwa upya na Shirika la Afya Duniani (WHO), na bado tunasubiri matokeo ya mwisho kuhusu hatua yetu ya Maturity Level 3.*

*Kwa kuzingatia kuwa mwaka huu tutakuwa na uchaguzi mkuu, tumeainisha mafanikio muhimu yaliyopatikana chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa kuwa sisi ni sehemu ya serikali iliyoko madarakani, chini ya Wizara ya Afya, tunalazimika kutoa taarifa kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala (yaani, CCM). Takwimu muhimu zimewekwa wazi ili kuonyesha kilichofanikishwa katika kipindi cha miaka minne chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.*

*Sambamba na kukamilika kwa utafiti wetu wa utoaji huduma (SDS), kiwango cha sasa cha kuridhika kwa wateja kimehesabiwa na kimeelezwa kwa muhtasari katika toleo hili. Vipengele vingine pia vinajumuisha maelezo kuhusu utendaji wa maabara yetu ya kisasa ya kudhibiti ubora (QC), msaada uliotolewa kwa kampuni zetu za ndani za kutengeneza dawa, kukamilika kwa jengo letu la ofisi kuu na mradi wa Mtambo wa kuteketeza taka (incinerator) huko Dodoma, matukio yanayoendelea katika ofisi zetu za kanda ikiwa ni pamoja na kuhamishwa kwa kanda ya kusini, na shughuli za udhibiti zilizofanyika kwa ajili ya kulinda afya ya jamii.*

*Kama sehemu ya kuimarisha ushirikiano na mashirika ya kimaendeleo kama WHO, Umoja wa Afrika (AU), jumuiya za kiuchumi za kikanda (RECs), na wadau wengine, tunaungana na Wizara ya Afya kumpongeza Profesa Mohammed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Kanda mpya wa WHO kwa Kanda ya Afrika. Nimemfahamu na kufanya kazi na Profesa Janabi kwa miaka mingi, na sina shaka kuwa atatekeleza majukumu yake mapya kwa mafanikio makubwa zaidi. Tunaahidi kumpa ushirikiano wote unaohitajika ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake mapya.*

*Kwa kumalizia, ningependa kukualika usome toleo hili, na iwapo kuna maoni, maboresho au mapendekezo yoyote, tafadhali usisite kuwasiliana nasi kupitia njia zetu za kawaida kwa ajili ya hatua stahiki.*

*Furahia kusoma Jarida lako!*

**Dkt. Adam Fimbo**
**Mkurugenzi Mkuu**

# TAHARIRI

***Mpendwa Msomaji Wetu,***

*Karibu kwenye toleo la 14 la Jarida la TMDA, jukwaa ambalo hutumika kuwasiliana, kutoa taarifa na kujadiliana na wewe mdau na mteja wetu wa thamani.*

*Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhariri Mkuu wa jarida hili, Dkt. Adam M. Fimbo, ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, kwa uongozi wake makini, msaada usiokoma, na mwongozo wake wa thamani uliowezesha maandalizi na kupitishwa kwa toleo hili.*

*Toleo hili limewasilishwa katika kipindi ambacho TMDA imepiga hatua kubwa za kitaasisi, huku taifa likiwa katika kipindi cha kutathmini maendeleo yake. Kadri Tanzania inavyojiandaa kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, tunakuletea muhtasari wa mafanikio muhimu yaliyofikiwa chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, pamoja na mchango wa TMDA katika kutekeleza vipaumbele vya Ilani ya Chama Tawala cha CCM. Kuanzia undaaji na utekelezaji wa Sera katika kulinda afya ya Wananchi.*

*Katika toleo hili, utapata makala mbalimbali zenye maudhui mbalimbali kuhusu maendeleo ya kiudhibiti, mafanikio ya miundombinu, ushirikiano wa kikanda, pamoja na mtazamo wa huduma kwa wateja. Taarifa zilizopo ni Pamoja na, namna TMDA ilivyoimarisha umihimu wake kimataifa kupitia Makubaliano ya Ushirikiano na Mamlaka ya Udhibiti ya Msumbiji, ushindi wa Tuzo ya Kampeni Bora ya Utoaji Elimu kwa Umma kwa mwaka 2024, pamoja na taarifa kuhusu kiwango cha kuridhika kwa wateja cha asilimia 75 ambayo ni ishara ya imani kubwa ya wadau wetu.*

*Pia nakukaribisha usome makala kuhusu mapinduzi ya uchunguzi wa dawa kupitia mashine ya kisasa ya LC-MS/MS, taarifa kuhusu maendeleo ya uzalishaji wa dawa ndani ya nchi, pamoja na tathmini ya jengo jipya la makao makuu ya TMDA na ujenzi wa tanuru la kuteketeza bidhaa zisizofaa uliokamilika jijini Dodoma.*

*Zaidi ya hayo, toleo hili linaonyesha kwa kina jinsi TMDA inavyotekeleza jukumu lake la kulinda afya ya jamii kupitia ukaguzi, uteketezaji wa dawa zisizofaa, na kampeni za uelewa kuhusu usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi yad awa na bidhaa bandia.*



*Mbali na taarifa za kitaalamu, jarida hili pia linaangazia matukio ya mshikamano, burudani na huduma kwa jamii kutoka kwenye michezo ya pamoja hadi kuwaaga wafanyakazi wastaafu yakikumbusha kuwa watu ndio kitovu cha mafanikio ya TMDA.*

*Natumaini toleo hili litakujulisha, litakuhamasisha, na kukuamsha kuchangia kwa dhati katika utekelezaji wa mamlaka yetu.*

*Maoni yako ni muhimu sana katika kuhakikisha tunaendelea kukufikishia taarifa kwa usahihi, uwazi na weledi.*

***Furahia usomaji!***



**Gaudensia Simwanza**
**Meneja, Mawasiliano na Elimu kwa Umma**

# TMDA Yasaini Makubaliano ya Ushirikiano na Mamlaka ya Udhibiti ya Msumbiji

*Mnamo Tarehe 7 Mei 2025, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dr. Adam Fimbo na Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania, Bw. Pedro Davane kwa niaba ya Serikali ya Msumbiji, walisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika eneo la udhibiti wa dawa kati ya mamlaka za udhibiti wa nchi hizi mbili.*

*Tukio hili la kihistoria lilifanyika Ikulu jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Mheshimiwa Daniel Francisco Chapo.*

*Makubaliano haya yalifikiwa wakati wa mazungumzo ya pande mbili kati ya Marais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Bw. Daniel Chapo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, yakilenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kati ya nchi hizi jirani.*

*Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema kuwa licha ya uhusiano wa kihistoria, kidiplomasia na kisiasa uliopo kati ya Tanzania na Msumbiji, ushirikiano wa kiuchumi umekuwa nyuma. Hivyo basi, nchi hizi mbili rafiki zimeamua kuimarisha ushirikiano wao hususan katika maeneo ya biashara na uchumi.*

*Makubaliano haya ni hatua muhimu inayoonesha dhamira ya dhati ya kurahisisha mifumo ya udhibiti wa dawa na kujenga uwezo wa kitaasisi kwa nchi zote mbili ili kutimiza majukumu yao ya kitaifa ya kulinda na kuendeleza afya ya jamii. MoU hii itaweka msingi wa ushirikiano wa karibu zaidi kati ya mamlaka hizo mbili katika maeneo ya usimamizi wa sekta ya dawa, kujengeana uwezo, kubadilishana taarifa, na kuoanisha mifumo ya udhibiti.*





*Makubaliano haya yanatarajiwa kuwezesha utekelezaji wa shughuli za udhibiti kwa pamoja ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa viwanda, uchunguzi wa maabara, ufuatiliaji wa usalama wa dawa (pharmacovigilance), pamoja na uanzishwaji wa viwango na miongozo ya pamoja. Vilevile, ushirikiano huu utasaidia programu za kubadilishana wataalamu na msaada wa kitaalamu kwa lengo la kukuza ubora na ubunifu katika udhibiti wa bidhaa za afya.*

*Akizungumza katika kikao hicho, Rais Chapo alieleza nia ya dhati ya Msumbiji kuimarisha ushirikiano wake na Tanzania, akibainisha kuwa Msumbiji imejaaliwa utajiri mkubwa wa rasilimali za asili.*

*Kwa upande wake, Rais Dkt. Samia alielezea ziara ya Rais Chapo kama uthibitisho wa urafiki wa muda mrefu na matarajio ya pamoja kati ya Tanzania na Msumbiji, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari.*

*Makubaliano haya ni hatua nyingine muhimu kuelekea utekelezaji wa malengo ya Shirika la Dawa la Afrika (AMA), yanayolenga kujenga viwango vya udhibiti vilivyooanika katika bara la Afrika.*

***Kwa upande wake, Rais Dkt. Samia alielezea ziara ya Rais Chapo kama uthibitisho wa urafiki wa muda mrefu na matarajio ya pamoja kati ya Tanzania na Msumbiji, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari***




# Miaka Minne ya Uongozi wa Rais Samia:TMDA yajivunia mafanikio

*Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, TMDA imepiga hatua kubwa na ya kupongezwa chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mamlaka imeimarisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kuhamasisha uzalishaji wa ndani, kuboresha utoaji wa huduma, na kuimarisha udhibiti wa bidhaa za afya.*

*Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam M. Fimbo, Mamlaka imekuwa na mchango mkubwa sana katika kusaidia mageuzi ya sekta ya afya na ajenda ya ukuaji wa viwanda chini ya uongozi wa Rais Samia. "Kupitia mageuzi ya kimkakati katika uwekezaji, tumeimarisha uwezo wetu wa udhibiti na kutoa mchango wa kutosha katika maendeleo ya afya na uchumi wa taifa," alisema Dkt. Fimbo.*

*Moja ya mafanikio makubwa yaliyoshuhudiwa ni kuwezesha uwekezaji wa viwanda 18 vya dawa na vituo 140 vya vifaa tiba na uchunguzi nchini, hatua iliyochochea uzalishaji wa ndani, uwekezaji na ajira.*

*Katika kipindi hicho, TMDA imesajili zaidi ya bidhaa 8,300 za dawa na zaidi ya bidhaa 3,000 za vifaa tiba na uchunguzi, kuhakikisha kuwa ni bidhaa zinazokidhi viwango vya juu vya usalama, ubora na ufanisi pekee ndizo zinazoidhinishwa kuingia sokoni. "Tunafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuwa ni bidhaa bora, salama na zenye ufanisi pekee ndizo zinazoingia sokoni, na hilo ndilo tumekuwa tukilisimamia kila siku," alisisitiza Dkt. Fimbo.*

*Mamlaka pia imeimarisha uwezo wake wa kifedha kwa kuongeza bajeti za kila mwaka na hivyo kuchangia kiasi cha takriban TZS bilioni 23.3 katika Mfuko mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miaka minne.*


*Uwekezaji wa zaidi ya TZS bilioni 15 katika vifaa vya kisasa vya maabara umeboresha uwezo wa kufanya maamuzi ya kiudhibiti kwa ushaidi wa kisayansi, na hivyo kuimarisha uangalizi wa udhibiti kwa ufanisi zaidi. Aidha, juhudi za kidijitali zimeboresha utoaji wa huduma, ambapo sasa mifumo ya kielektroniki ya utoaji vibali ina uwezo wa kutoa kibali ndani ya saa 24 pekee.*

*Katika kipindi hicho, TMDA imeendelea kutekeleza viwango vya kimataifa kwa kudumisha cheti cha ISO 9001:2015 na ithibati ya maabara chini ya ISO/IEC 17025:2017. Zaidi ya hapo, maabara ya TMDA imeendelea kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), ambapo maabara ya kupima dawa imeendlea kutambuliwa na WHO tangu mwaka 2011. Maabara ya microbiolojia ilipata hadhi hiyo mwaka 2022, na maabara ya vifaa tiba imepata Ithibati kwa kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 mwaka 2024.*

*Kwa sasa, zaidi ya asilimia 98 ya bidhaa zinazodhibitiwa nchini zinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa, na hivyo kulinda afya ya jamii na kuongeza imani ya watumiaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi. Wakati huohuo, usimamizi wa bidhaa baada ya kuingia sokoni (PMS) umeimarishwa, ambapo idadi ya vituo vya kufuatilia madhara ya dawa na chanjo imeongezeka hadi kufikia 30 nchi nzima. Mamlaka pia imeongeza mtandao wa maabara hamishika kutoka 19 hadi 28 ili kuwezesha ukusanyaji na upimaji wa sampuli kwa ufanisi katika maeneo mbalimbali.*

*Vilevile, TMDA imeendeleza miundombinu yake kwa kupanua ofisi ya Makao Makuu na kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Tanuru jijini Dodoma kwa ajili ya kuteketeza bidhaa duni, bandia au zisizofaa kwa matumizi. Kwa uwiano, idadi ya wafanyakazi wa TMDA imeongezeka kutoka 278 hadi 421, jambo linalodhihirisha ukuaji wa taasisi katika rasilimali watu na uwezo wa kitaasisi.*

*"Hatua hizi ni kielelezo cha dhamira yetu ya kulinda afya ya umma, kuunga mkono ajenda ya maendeleo ya taifa, na kutekeleza malengo yaliyowekwa katika Ilani ya Chama Tawala," alihitimisha Dkt. Fimbo.*



# Naibu Waziri Aitaka MAB Kuboresha Upatikanaji wa Dawa Bora na Nafuu

*Katika juhudi za kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania, Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mb), alikutana na Bodi ya Ushauri ya Wizara (MAB) tarehe 21 Februari, 2025, jijini Arusha.*

*Mkutano huo uliitishwa kwa lengo la kufanya tathmini ya utendaji wa TMDA katika kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha upatikanaji wa bidhaa za afya bora, salama na nafuu kwa wananchi. Miongoni mwa mambo yaliyogusiwa ni pamoja na bei kubwa za dawa, ambazo ziliibuliwa na wadau mbalimbali.*

*"Kazi kubwa iliyo mbele yenu ni kupitia mifumo ya kutoa idhini ya uingizaji wa bidhaa za afya sokoni ili kupunguza gharama zinazowakumba waagizaji na wazalishaji, ambazo hatimaye huwalemea watumiaji," alisema Dkt. Mollel, huku akiwataka wajumbe wa MAB kushirikiana kwa karibu na Uongozi wa TMDA katika kuboresha na kurahisisha taratibu za udhibiti.*

*Aidha, aliongeza kuwa kuna umuhimu kwa Mamlaka kuangalia namna bora ya kuunda mazingira rafiki kwa wazalishaji wa ndani, ili kuchochea uwekezaji katika sekta ya dawa na vifaa tiba. Hatua hii inalenga kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi na hivyo kuongeza upatikanaji wa dawa.*

*"Nafahamu Mamlaka inaendelea kutekeleza mpango wa kujenga uwezo wa wazalishaji wa ndani. Kazi kubwa imefanyika tayari, ambapo viwanda vya dawa vimeongezeka nchini, lakini bado tunahitaji juhudi zaidi, ikizingatiwa haja ya kupunguza utegemezi wa dawa kutoka nje," alieleza Dkt. Mollel.*

*Kwa upande mwingine, Dkt. Mollel aliipongeza TMDA kwa juhudi inazoendelea kuzifanya katika kulinda afya ya umma kwa kuhakikisha kuwa dawa, vifaa tiba na vipimo vyote vinavyosambazwa vinakidhi viwango vya ubora, usalama na ufanisi. Alisisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi hizo huku akihimiza ubunifu wa njia za kupunguza bei za dawa bila kuathiri ubora wake.*

*Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Ushauri, Mwenyekiti wake, Bw. Eric Shitindi, alihakikishia kuwa Bodi itaendelea kuunga mkono TMDA kwa kutoa miongozo ya kimkakati na usimamizi.*

*"Bodi itaendelea kutumia utaalamu wake kitaaluma kuiongoza TMDA katika kujielekeza kwenye vipaumbele vya kitaifa na kuboresha ufanisi wa utendaji," alieleza Bw. Shitindi.*

*Vilevile, maelekezo ya Naibu Waziri yanaendana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha afya ya jamii kwa kuongeza upatikanaji wa bidhaa za afya za uhakika na nafuu.*

*Mkutano ulifungwa kwa makubaliano ya pamoja kuwa mfumo Madhubuti katika udhibiti ni muhimu katika kufanikisha huduma za afya kwa wote na kuimarisha imani kwa sekta ya afya nchini.*

# TMDA Yakamilisha Upanuzi wa Ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma

*TMDA imekuwa ikijitahidi kwa dhati kutoa huduma bora za udhibiti kwa wadau wake na jamii kwa ujumla, kwa lengo la kukidhi mahitaji na matarajio yao ya kila siku. Kwa kipindi cha miaka kadhaa, Mamlaka imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wake na pia kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wateja wake.*

*Kwa kuzingatia dira yake ya kuhakikisha huduma inawafikia wananchi na kupunguza gharama zisizo za lazima pamoja na usumbufu kwa wateja, TMDA imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya miundombinu. Hasa, Mamlaka imekuwa ikitumia mapato ya ndani yanayotokana na ada na tozo mbalimbali za huduma katika kujenga majengo ya ofisi yanayosaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.*

*Moja ya mafanikio makubwa katika juhudi hizi ni kukamilika kwa awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la ofisi ya makao makuu ya TMDA jijini Dodoma. Awamu ya kwanza ya mradi huu ilihusisha ujenzi wa jengo la ghorofa mbili ambapo Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilikuwa mkandarasi mkuu na ABECC walikuwa washauri wa mradi. Awamu hii ya kwanza ilikamilika kwa mafanikio mwezi Juni 2021.*

*Wakati huo, jengo hilo lililotangulia kujengwa lilitumika kwa shughuli mbalimbali muhimu ikiwa ni pamoja na maabara ya kupima bidhaa za mitishamba na tumbaku, Ofisi ya Kanda ya Kati na ofisi ya makao makuu ya TMDA.*

*Hata hivyo, kutokana na ongezeko la idadi ya watumishi na kupanuka kwa wigo wa majukumu ya TMDA, kulijitokeza uhitaji wa dharura wa kuongeza nafasi ya ofisi. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka ilianza mchakato wa upanuzi wa jengo hilo mwaka 2023 kwa kumtumia mkandarasi Hainan International Construction Company ambaye aliongeza ghorofa mbili juu ya jengo lililokuwepo.*

*Mradi huu sasa umekamilika, na tunatoa shukrani za dhati kwa mshauri na mkandarasi kwa kutekeleza jukumu hili kwa mafanikio. Bodi ya Ushauri ya Wizara pia tunaishukuru kwa kusimamia mradi huu kutoka mwanzo hadi mwisho. Vilevile, wasimamizi wote wa mradi ndani ya TMDA akiwemo Kaimu Meneja wa Manunuzi Bi. Donatha Koko na Mkaguzi wa Kazi Bw. Baraka Chacha wanapongezwa kwa juhudi zao kubwa hadi kufikia hatua hii. Mwisho, timu ya Menejimenti inashukuriwa kwa usimamizi wa karibu na uidhinishaji wa hatua zote muhimu zilizowezesha kukamilika kwa mafanikio kwa mradi huu.*




TMDA Completes Expansion of its Headquarter Offices in Dodoma

# Mafanikio Makubwa Uwekezaji viwanda vya Dawa: Uongozi wa TMDA Watembelea Viwanda vya Ndani



*Katika kuharakisha jitihada za Tanzania kufikia azma yake ya kuongeza uzalishaji wa dawa na kukuza uchumi wa viwanda, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Mitangu Fimbo, aliongoza ziara ya kimkakati ya ukaguzi wa viwanda vya uzalishaji wa dawa katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuanzia tarehe 24 hadi 28 Machi, 2025.*

*Ziara hiyo ilikuwa sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kukuza Uzalishaji wa Ndani wa Bidhaa za Afya (2022/23–2026/27), ambapo lengo kuu lilikuwa ni kuimarisha usimamizi wa viwanda vya dawa kwa kutathmini uwezo wa uzalishaji, kubaini fursa za kuboresha udhibiti, pamoja na maeneo yanayohitaji msaada wa kitaalamu zaidi.*

*Katika ziara hiyo, timu ya Menejimenti ya TMDA ilitembelea jumla ya viwanda tisa (9) vya ndani vinavyozalisha bidhaa za dawa ambapo kati yake viwanda vinane (8) vinazalisha dawa za binadamu na kimoja (1) huzalisha chanjo za mifugo.*

> **TMDA inaamini kuwa kuunga mkono uzalishaji wa ndani ni msingi wa kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa bora, salama na nafuu kwa Watanzania wote," alisema Dkt. Fimbo akiwa katika moja ya viwanda.**

*Viwanda vilivyotembelewa ni Alfa Pharmaceuticals Ltd, Cure Afya Pharmaceuticals Ltd, Mansoor Daya Chemicals, Keko Pharmaceuticals Industries (KPI) Ltd, Zenufa Laboratories Ltd, Shelys Pharmaceuticals Ltd, Katwaza Pharmaceuticals Ltd, Kairuki Pharmaceuticals Ltd, na Hester Biosciences Africa ambayo huzalisha chanjo za mifugo.*

*Dkt. Fimbo na timu yake walifanya majadiliano ya kina na ya kutafuta suluhisho ya Pamoja kwa wamiliki wa viwanda, wataalamu wa uzalishaji, wahakiki wa ubora (QA), na udhibiti wa ubora (QC).*

*Mjadala ulijikita kwenye mikakati ya kuongeza uzalishaji, kuzingatia viwango bora vya uzalishaji vya kimataifa, kuzingatia matakwa ya kisheria, kuboresha miundombinu pamoja na ujuzi wa wafanyakazi.*


*Ushirikiano ulioonekana wakati wa ziara hiyo unadhihirisha dhamira ya TMDA kuwa siyo msimamizi tu, bali pia mwezeshaji wa ubunifu na maendeleo ya viwanda katika sekta ya afya ya Tanzania.*

*"TMDA inaamini kuwa kuunga mkono uzalishaji wa ndani ni msingi wa kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa bora, salama na nafuu kwa Watanzania wote," alisema Dkt. Fimbo akiwa katika moja ya viwanda.*

*Mbali na kutathmini uzingatiwaji wa viwango vya kitaifa na kimataifa, ziara hiyo pia ilitoa fursa ya kutoa mwongozo wa kitaalamu unaolenga kuboresha ufanisi wa uendeshaji, kuongeza uwezo wa uzalishaji na kubaini maeneo yanayohitaji uwekezaji katika teknolojia za kisasa za uzalishaji wa dawa.*


*Aidha, ziara hiyo iliimarisha dhamira ya kimkakati ya TMDA katika kuendeleza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, pamoja na kuongeza uwezo wa nchi kukidhi mahitaji ya soko la ndani na la kikanda kupitia uzalishaji wa ndani.*

*Kupitia hatua hii, TMDA inaweka mwelekeo wa wazi kuelekea kwenye tasnia thabiti na yenye kujitegemea ya dawa, yenye uwezo wa kulinda afya ya jamii sambamba na kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya uchumi wa taifa.*










# Bidhaa Bandia Zakamatwa huku TMDA ikiimarisha Juhudi za Kulinda Afya ya jamii

*TMDA kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usimamizi wa sheria, imeimarisha nguvu katika kudhibiti usambazaji wa dawa bandia na zisizokidhi viwango kupitia operesheni maalum ya ukaguzi iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 8 Novemba, 2024.*

*Operesheni hiyo ililenga kudhibiti dawa tiba zenye asili ya kulevya katika kanda tano kati ya nane za TMDA.*

*Mbali na TMDA, taasisi nyingine zilizoshiriki kwenye operesheni hiyo ni pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Baraza la Famasi Tanzania, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), na Bohari ya Dawa (MSD).*

*Katika kipindi hicho cha operesheni, jumla ya vituo 116 ikiwemo hospitali, maduka ya dawa, waingizaji na wasambazaji wa bidhaa za afya vilikaguliwa ili kubaini utii wao kwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura 95, na Sheria ya Viwandani na Kemikali kwa Matumizi ya Binadamu Sura 182.*

*Kati ya vituo vilivyokaguliwa, 24 sawa na asilimia 20.7 vilibainika kukiuka sheria tajwa. Kati ya hivyo, vituo vitano (4.3%) vilionesha dalili za kupotea au kuhamishwa kwa dawa za kulevya isivyo halali.*

*Aidha, vituo 10 (8.6%) vilikutwa na dosari katika utunzaji wa kumbukumbu, na vituo sita (5.2%) vilikuwa na maeneo ya kuhifadhia dawa ambazo hazikukidhi masharti ya kuhifadhi dawa za kudhibitiwa.*

*Kituo kimoja (0.9%) kilishindwa kuripoti upotevu wa dawa za kulevya kwa TMDA, jambo ambalo ni ukiukwaji mkubwa wa maadili ya usimamizi wa dawa hizo.*

*Zaidi ya hayo, dawa na vifaa tiba ambavyo havijasajiliwa vilikamatwa katika hospitali 13, maduka ya dawa sita, na kituo kimoja cha forodha.*

*Thamani ya bidhaa zilizokamatwa inakadiriwa kufikia zaidi ya Shilingi milioni 18, ambapo dawa pekee ziligharimu Shilingi milioni 17.6 na vifaa tiba viligharimu Shilingi 393,200.*

*TMDA inaendelea kuimarisha mifumo yake ya udhibiti kwa lengo la kulinda afya ya jamii.*

*Mamlaka inatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa kuhusu vitendo visivyofaa na haramu vinavyohatarisha afya ya jamii kupitia njia rasmi za mawasiliano za TMDA.*

***Thamani ya bidhaa zilizokamatwa inakadiriwa kufikia zaidi ya Shilingi milioni 18, ambapo dawa pekee ziligharimu Shilingi milioni 17.6 na vifaa tiba viligharimu Shilingi 393,200. TMDA inaendelea kuimarisha mifumo yake ya udhibiti kwa lengo la kulinda afya ya jamii.***



# LC-MS/MS –Mashine Inavyoleta mageuzi katika Uchunguzi wa Dawa

*TMDA imepiga hatua kubwa katika uchunguzi wa dawa kupitia matumizi ya kifaa cha kisasa cha Liquid Chromatography Tandem Mass Spectrometry/Mass Spectrometry (LC-MS/MS).*

*Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Huduma za Maabara wa TMDA, Dkt. Danstan Hipolite Shewiyo, upatikanaji wa kifaa hiki cha LC-MS/MS umeleta mapinduzi makubwa katika uchunguzi wa dawa, hasa katika kubaini uchafuzi wa viambata hatarishi kama diethylene glycol, ethylene glycol, na nitrosamines – ambavyo vina madhara makubwa kiafya.*

*"Teknolojia hii inatuwezesha kuchambua mchanganyiko tata wa dawa kwa usahihi wa hali ya juu na kwa kasi ya kipekee," alisema Dkt. Shewiyo katika mahojiano ya hivi karibuni.*

*Dkt. Shewiyo aliongeza kuwa matumizi ya LC-MS/MS katika maabara za TMDA zilizoko Dar es Salaam na Mwanza yameongeza uwezo wa Mamlaka kusaidia kulinda afya ya jamii.*

*Hospitali, wazalishaji wa dawa, na taasisi za utafiti kote nchini Tanzania wanaweza kunufaika na huduma za uhakika za uchunguzi wa maabara zinazotolewa na TMDA.*

*Teknolojia hii ya kisasa kabisa inabadilisha namna dawa zinavyochunguzwa nchini, na kuimarisha nafasi ya TMDA kama chombo kinachoongoza katika udhibiti wa dawa barani Afrika.*

*LC-MS/MS ni teknolojia ya utambuzi wa masi (mass spectrometry) inayotumia mfumo wa triple quadrupole mass analyzer kutambua na kupima viambata katika sampuli mbalimbali, ikiwemo dawa, vyakula, na kemikali, kwa usahihi wa hali ya juu.*

*Inafanya kazi kwa kutenganisha ioni kulingana na uwiano wao wa mass-to-charge (m/z), na kuruhusu tu ioni zenye sifa zinazotakiwa kupita kwenye vijiti vya quadrupole. Utaratibu huu huchuja ioni ili kuhakikisha kwamba ni zile tu zenye sifa stahiki ndizo zinazogunduliwa na kuchambuliwa.*

*Kiini cha thamani ya mashine hii ni uwezo wake mkubwa wa kutambua viambata kwa hisia (sensitivity) na uchambuzi (selectivity) wa hali ya juu. Inaweza kugundua uchafu kwa kiwango cha chini sana katika sampuli tata, kutambua viambata vinavyojulikana na visivyojulikana, na kutoa data ya ubora (qualitative) na kiasi (quantitative).*

*Cha muhimu zaidi, mashine hii hutoa matokeo kwa haraka bila ya kuhitaji uthibitisho wa muda wa kushikiza (retention), jambo linalopunguza sana muda na rasilimali zinazotumika katika uchambuzi.*

*Uimara wa LC-MS/MS pia unaifanya kuwa bora kwa mazingira ya maabara ya TMDA. Imesanifiwa kushughulikia sampuli chafu ("dirty samples"), ni rahisi kusafisha na kutunza, na hivyo kuongeza ufanisi na umahiri wake.*

*Zaidi ya hayo, mashine hii inaweza kufanya kazi kwa kujitegemea ikiwa na mfumo wa ndani wa kuhakikisha nishati ya umeme inapatikana muda wote, hata wakati wa mabadiliko ya nguvu za umeme.*

*Mbali na uchunguzi wa dawa, maabara za TMDA zimeweka vifaa vya kisasa kwa ajili ya kusafisha na kuua vijidudu katika mavazi ya hospitali kama aproni, magwanda, na vifaa vingine muhimu, na hivyo kuchangia usalama zaidi katika mazingira ya matibabu.*

*Kupitia uwekezaji endelevu katika miundombinu, teknolojia, na rasilimali watu, TMDA inalinda afya ya jamii huku ikijenga mfumo imara wa udhibiti wa dawa nchini.*





# Wizara ya Afya Yaunda Kikosi Kazi cha Uteketezaji Salama wa Vifaa Tiba Visivyotumika

> **Kwa upande mwingine, Bi. Joyce Chuwa, akizungumza kwa niaba ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, alisisitiza umuhimu wa kuteketeza vifaa tiba kwa wakati na kwa usalama ili kuepuka madhara ya kiafya kwa jamii. Alifafanua kuwa, "Kikosi kazi kinapaswa kusimamia na kufuatilia vifaa tiba vingi na vikubwa ambavyo havitumiki katika vituo vya afya vya umma na binafsi."**

*Ili kukabiliana na ongezeko la vifaa tiba visivyotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara ya Afya imeunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kuratibu na kurahisisha uteketezaji wa vifaa tiba ambavyo havifai kwa matumizi.*

*Kikosi hicho kiliundwa katika kikao kilichofanyika tarehe 30 Aprili, 2025 katika Makao Makuu ya TMDA jijini Dodoma.*

*Akizindua rasmi Kikosi Kazi hicho, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, alihimiza wanachama wa kikosi hicho kufanya mikutano ya mara kwa mara ili kutathmini hali halisi na kupanga mikakati ya haraka ya kuteketeza vifaa tiba visivyotumika vilivyopo katika vituo vya afya vya umma na binafsi kote nchini.*

*Kikosi Kazi hicho, ambacho kitaongozwa na Wizara ya Afya, kinajumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), pamoja na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi (PHAB).*

*Kwa upande mwingine, Bi. Joyce Chuwa, akizungumza kwa niaba ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, alisisitiza umuhimu wa kuteketeza vifaa tiba kwa wakati na kwa usalama ili kuepuka madhara ya kiafya kwa jamii.*

*Alifafanua kuwa, "Kikosi kazi kinapaswa kusimamia na kufuatilia vifaa tiba vingi na vikubwa ambavyo havitumiki katika vituo vya afya vya umma na binafsi."*

*Kikosi kazi hicho kinatarajiwa kukamilisha jukumu lake ndani ya kipindi cha miezi sita, kuanzia Aprili 2025, kama ilivyoelekezwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).*



# Awamu ya Kwanza Mradi wa ujenzi wa Tanuru yakamilika

*Awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa Tanuru kwa ajili ya kuteketeza dawa, vifaa tiba na vitendanishi visivyofaa kwa matumizi pamoja na taka za tiba, ulioanza mwaka 2024, hatimaye umekamilika.*

*Hii ni mojawapo ya mafanikio makubwa ya TMDA ikilenga kuhakikisha usalama na ulinzi wa mazingira katika uteketezaji wa bidhaa tiba zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.*

*Kufuatia kukamilika kwa awamu hii, tarehe 7 Oktoba 2024 TMDA ilifanya hafla fupi ya makabidhiano rasmi ya mradi huu uliojengwa katika eneo la Nala, Mkoa wa Dodoma, ambapo Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa TMDA (MAB), Bw. Eric Shitindi alipokea mradi huu kwa niaba ya Wizara.*

*Makabidhiano hayo yalishuhudiwa na menejimenti ya TMDA, mkandarasi (National Housing Corporation – NHC), na mtaalam mshauri (ABECC), ambapo Mwenyekiti wa Bodi alikabidhiwa Cheti kama ishara ya kukamilika rasmi kwa mradi huo.*



*Hatua hii inadhihirisha maendeleo makubwa katika miundombinu ya afya nchini Tanzania, ambapo tanuru hili litakapoanza kufanya kazi litahusika na uteketezaji na uondoaji wa bidhaa za afya zisizofaa kama vile bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi, zilizokamatwa wakati wa ukaguzi, zisizosajiliwa, na zile zilizothibitishwa kuwa bandia au duni.*

*Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa MAB, Bw. Eric Shitindi alisema Tanuru hili litahakikisha kuwa bidhaa zote za afya zisizofaa kwa matumizi ya binadamu na mifugo zinateketezwa kwa usalama na bidhaa bora, salama, na zenye ufanisi pekee ndizo zinazozunguka sokoni."*

*Tanuru hili linatarajiwa kuwa kitovu cha uteketezaji kwa kuwa linafikika na wadau mbalimbali kote nchini kwa urahisi. Aidha, litasaidia kuokoa takribani shilingi milioni 150 kila mwaka ambazo TMDA inatumia kama ada za kuteketeza bidhaa katika vituo vya kibinafsi.*

*Awamu ya kwanza ya mradi huu ilihusisha ujenzi wa ghala la kuteketeza, ukuta wa kiusalama wa ghala, kisima cha maji na jumba la ghala. Awamu ya mwisho itahusisha usimikaji wa mtambo wa kuteketeza, mifumo ya usalama, na huduma nyingine za msaada.*

*TMDA imejipanga kukamilisha awamu ijayo ya mradi huu wa tanuru ikiwa ni mkakati wa kuboresha mifumo ya afya na kulinda Watanzania dhidi ya hatari zinazotokana na bidhaa za afya zilizoteketezwa au kutupwa bila kufuata utaratibu.*

# Maabara ya TMDA Yaendelea Kuhakikisha Ubora na Usalama wa Bidhaa za Afya



*TMDA inaendelea kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa za afya nchini kupitia maabara yake ya kisasa kabisa, ambayo sasa ina uwezo wa kufanya zaidi ya asilimia 95 ya vipimo vya ubora kwa bidhaa zote zinazodhibitiwa za afya.*

*Hatua hii ni mafanikio makubwa yanayoashiria ongezeko la uwezo wa taifa katika kulinda afya ya jamii na kuhakikisha ubora na usalama wa dawa, vifaa tib ana vitendanishi.*

*"Haya ni mafanikio ya kipekee kwa maabara ya TMDA na yanaifanya kuwa miongoni mwa maabara bora kabisa za udhibiti barani Afrika," alisema Dkt. Danstan Shewiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Maabara, wakati wa mahojiano ya hivi karibuni.*

*"Ninapenda Watanzania watambue kuwa Maabara ya TMDA inafanya kazi kwa kiwango cha juu kabisa cha taaluma na usahihi, ikitoa matokeo ya vipimo ya kuaminika yanayoiwezesha Mamlaka kufanya maamuzi sahihi ya udhibiti kwa lengo la kulinda afya ya jamii," alisisitiza Dkt. Shewiyo.*

*TMDA inaendesha maabara katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, na Dodoma, ambapo kila moja ina eneo maalum la kipaumbele. Maabara ya Dar es Salaam inahusika na uchunguzi wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi. Maabara ya Mwanza inajikita katika bidhaa za dawa na utafiti, huku ile ya Dodoma ikishughulikia uchunguzi wa bidhaa za tumbaku na dawa za tiba asili.*

*Maabara hizo zimewekewa vifaa vya kisasa vya teknolojia ya juu, vinavyowezesha uchunguzi wa kina wa malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa dawa za binadamu, mifugo, na dawa za asili.*

*Vipimo vinavyofanywa ni pamoja na utambuzi wa viambato hai, upimaji wa nguvu ya dawa (assay), kiwango cha unyevu, na uchambuzi wa uchafu hatarishi kama vile diethylene glycol, ethylene glycol, na nitrosamines.*

*Mbali na vipimo vya ubora, maabara za TMDA pia hupima ubora wa vifungashio, hufanya tafiti mbalimbali, na kutekeleza majukumu mengine kama yalivyoelekezwa na Mamlaka.*

*Kwa mujibu wa Dkt. Shewiyo, matokeo yanayotolewa na maabara hizo ni ya msingi sana katika maamuzi ya udhibiti ya TMDA, kwani yanatokana na takwimu za kisayansi za kina.*

*Maabara hupokea sampuli kutoka vyanzo viwili vikuu: sampuli za bidhaa zinazodhibitiwa (regulatory), zinazokusanywa kwa madhumuni ya maamuzi ya TMDA, na sampuli zisizo za kiudhibiti (non-regulatory), zinazowasilishwa na wadau kama wazalishaji na watafiti kwa ajili ya uthibitisho wa ubora wa bidhaa.*

*Sampuli za bidhaa zinazodhibitiwa hutoka ndani ya idara za TMDA, ambazo huwasilisha bidhaa kwa ajili ya usajili, ukaguzi, na ufuatiliaji wa soko. Sampuli zisizo za kiudhibiti huwasilishwa na wazalishaji wa ndani na wa kimataifa, watafiti, au taasisi mbalimbali zinazohitaji uthibitisho wa ubora.*

*Akizungumzia maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Dkt. Shewiyo alitaja mafanikio kadhaa makubwa: maabara ya kemia imeendelea kutambuliwa na WHO tangu mwaka 2011; maabara ya microbiolojia ilipata utambuzi wa WHO mwaka 2022; na maabara ya vifaa tiba ilipata cheti Ithibati kwa kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 mwaka 2024.*

*Aidha, Dkt. Shewiyo alitambua mchango wa Serikali kwa kushirikiana na wafadhili wa kimataifa katika kusaidia maendeleo ya maabara hiyo. "Kupitia msaada kutoka Global Fund, tumepata vifaa vya kisasa vyenye thamani ya takriban TZS bilioni 10 za Kitanzania kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kupima chanjo za binadamu na dawa za kibaolojia," alieleza.*

*Uwekezaji unaoendelea wa TMDA katika miundombinu ya maabara, vifaa vya kisasa, na rasilimali watu ni ushahidi wa dhahiri wa dhamira yake ya kuendeleza ubora katika udhibiti wa bidhaa za afya. Mamlaka inavyozidi kupanua wigo wa shughuli zake, inabakia kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata bidhaa za afya zilizo salama, bora, na zenye ufanisi.*



# TMDA Yashinda Tuzo ya Kampeni Bora ya Utoaji Elimu kwa Jamii

*Kama ishara inayosisitiza nguvu ya ushirikishwaji bora wa jamii, TMDA imetunukiwa Tuzo ya Kampeni ya Utoaji Elimu Bora kwa Umma ya 2024.*

*Tuzo hii ilitolewa wakati wa hafla maalum ya utoaji tuzo za Public Relations & Communication Excellence Awards iliyofanyika tarehe 3 Aprili, 2025, jijini Dar es Salaam.*

*Tuzo hii si tu ya heshima ya mafanikio, bali ni ishara ya juhudi kubwa za TMDA katika kuboresha namna Watanzania wanavyoelewa, kuwasiliana na kujilinda kupitia matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba.*

*Katika chimbuko la kampeni hii iliyoshinda tuzo, kulikuwa na lengo moja kuu na lenye kugusa jamii ambalo lilihusu kuwawezesha wananchi kuripoti madhara au maudhi yanayotokana na dawa wanazotumia. Kupitia matumizi ya vyombo vya habari vya kitaifa, mikutano ya mihadhara, mitandao ya kijamii, na ushirikiano na vituo vya afya, TMDA ilianzisha kampeni ya kitaifa iliyowahamasisha wananchi kuchukua jukumu la afya zao kwa kuripoti madhara yatokanayo na matumizi ya dawa (ADRs).*

*Matokeo yake yamekuwa ya kuvutia. Kutoka wastani wa taarifa 200 za madhara kwa mwaka kabla ya kampeni, sasa TMDA inapokea zaidi ya taarifa 8,000 kila mwaka ongezeko la zaidi ya mara 40. Mwitikio huu unaonyesha ongezeko la uelewa na umakini miongoni mwa umma, pamoja na mabadiliko ya kimtazamo ambapo watu sasa wanashiriki kikamilifu kulinda siyo tu afya zao, bali pia za jamii zao.*

*Mchango wa taarifa hizi umevuka mipaka ya Tanzania. Nchi sasa imechangia jumla ya taarifa 62,038 za matukio kwenye kanzidata ya kimataifa ya ufuatiliaji wa usalama wa dawa (Vigibase) inayoendeshwa na WHO, ambayo ni sawa na 0.2% ya taarifa zote duniani. Mchango huu mkubwa umeiweka Tanzania katika nafasi ya 47 kati ya nchi 168, hivyo kuipa nafasi ya kipekee kwenye ramani ya dunia katika ufuatiliaji wa usalama wa dawa.*

*Ndani ya kila taarifa kuna tukio linalogusa jamii: mama anayeona mabadiliko ya ajabu kwa mtoto wake, muuguzi anayemwelekeza mgonjwa wake kutoa taarifa, au kijana anayetumia mitandao ya kijamii kuonyesha uzoefu wake. TMDA ilihakikisha kuwa sauti hizi zinasikika na kuthaminiwa.*

*"Tuzo hii ni ushuhuda wa nguvu ya wananchi," alisema Dkt. Yonah H. Mwalwisi, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa wa TMDA, muda mfupi baada ya kupokea tuzo hiyo kwa niaba ya taasisi. "Ni utayari wao wa kujifunza, kuripoti, na kulindana ndio ulioleta mafanikio haya. Wajibu wetu ni kuendelea kuwaongoza kwa maarifa na msaada," aliongeza Dkt. Yonah.*

*Aidha, Dk. Yonah alitanabaisha kuwa, mafanikio ya kampeni hii yanatufundisha kuwa elimu ya afya ya umma si tu kutoa taarifa; bali ni kuwawezesha watu. Jamii iliyoelimika husababisha matumizi salama ya dawa, vifaa tiba vinavyoaminika, na mfumo wa afya ulio imara na unaodumu.*

*TMDA inaposherehekea kutambuliwa kitaifa, ujumbe unabaki wazi: elimu huokoa maisha, na kila taarifa ina umuhimu wake.*





# Wagonjwa wa Saratani Hospitali ya Bugando Warejeshewa tabasamu: Shukrani kwa Watumishi Wanawake wa TMDA

*Katika kueendelea na maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi 2025, watumishi wanawake wa TMDA walitembelea na kutoa msaada wa vifaa vya usafi kwa wagonjwa wa saratani wanaopatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando, iliyopo Mwanza.*

*Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo tarehe 4 Aprili 2025, kama sehemu ya mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa, Bi. Sophia Mziray, alisisitiza kuwa Mamlaka inatambua changamoto wanazokutana nazo wagonjwa wa saratani na watoa huduma zao, na kwamba imeamua kutoa msaada huu ili kurahisiha huduma na kupunguza mateso.*

*"Saratani inahitaji matibabu ya muda mrefu, na ni gharama kubwa. Tumekuja hapa kushirikiana na Watanzania wenzetu. Tunaamini msaada huu utarudisha tena furaha yao na kuleta tabasamu angalau kwa muda," alieleza Bi. Mziray.*

*Akipokea msaada huo, Mkurugenzi wa Huduma za Afya katika Hospitali ya Bugando, Dkt. Cosmas Mbulwa, aliwashukuru watumishi wanawake wa TMDA kwa msaada wao.*

*"Ni kweli kuwa matibabu haya yanachukua muda mrefu na ni ya gharama kubwa, watanzania wenzetu wanahitaji faraja, huduma, na msaada wa mara kwa mara. Nina uhakika kuwa wagonjwa wetu watajisikia vizuri na kuona wamethaminiwa kupitia msaada huu kutoka TMDA," alisema Dkt. Mbulwa.*

*Dkt. Mbulwa aliongeza kuwa, "Hospitali ya Bugando inapokea wagonjwa wa saratani kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na maeneo mengine. Misaada ya aina hii inahitajika sana kwa watoa huduma na wagonjwa. Tunapokea msaada wowote, iwe wa aina ya vitu au vinginevyo, na tunaomba wadau wengine kuiga mfano huu ili kuwasaidia wagonjwa wa Bugando."*

*Wanawake kote nchini waliungana na wenzao duniani kote kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi. Nchini Tanzania, maadhimisho ya kitaifa yalifanyika jijini Arusha, ambapo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.*

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango akimsikiliza Dkt. Adam Fimbo, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, wakati wa uwasilishaji wake kuhusu mchango wa TMDA katika afya ya Jamii kwenye maonesho ya Mkutano Mkuu wa Chama cha Wanataaluma wa Dawa Tanzania (PST) tarehe 4 Juni 2025 jijini Arusha.*



*Picha ya pamoja ya maafisa wa TMDA na maafisa watatu wa TEHAMA kutoka Mamlaka ya Dawa ya Ghana (Ghana FDA) wakati wa ziara yao ya kujifunza kuhusu Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Udhibiti (RIMS) katika TMDA, iliyofanyika kuanzia Mei 26 hadi 30, 2025, mjini Dodoma.*




*Balozi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri nchini Tanzania, Mhe. Balozi Sherif Ismail, katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa TMDA wakati wa ziara yake katika Mamlaka hiyo tarehe 15 Mei 2025 jijini Dar es Salaam, iliyolenga kujadili ushirikiano wa udhibiti na kuimarisha uhusiano wa pande mbili.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Balozi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri nchini Tanzania, Mhe. Balozi Sherif Ismail, alikutana na Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, tarehe 15 Mei 2025 jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili ushirikiano wa kisheria katika udhibiti na kuimarisha uhusiano wa pande mbili katika sekta ya afya.*



*Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, akiwa pamoja na Dkt. Yonah Mwalwisi, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa, na Bw. Adonis Bitegeko, Meneja wa Kanda ya Mashariki ya TMDA, walitembelea Kiwanda cha Dawa cha Katwaza kilichopo Mkoa wa Pwani tarehe 27 Machi 2025 kwa ajili ya kujadili changamoto zinazohusiana na usajili wa dawa nchini Tanzania.*



*Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, pamoja na Dkt. Yonah Mwalwisi, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa, na Bw. Adonis Bitegeko, Meneja wa Kanda ya Mashariki ya TMDA, walitembelea Kiwanda cha Dawa cha Katwaza kilichopo Mkoa wa Pwani tarehe 27 Machi 2025 kwa ajili ya kujadili changamoto zinazohusiana na usajili wa dawa nchini Tanzania.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, alitembelea Kiwanda cha Alfa Pharmaceuticals jijini Dar es Salaam tarehe 25 Machi 2025 kwa ajili ya kushughulikia changamoto za usajili wa dawa na kutoa msaada wa kitaalamu. Aliambatana na Dkt. Yonah Mwalwisi, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa, pamoja na Bw. Adonis Bitegeko, Meneja wa Kanda ya Mashariki wa TMDA.*



*Tarehe 28 Februari 2025, TMDA ilikabidhi kwa fahari kompyuta mpakato mbili kwa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala (KIU) kampasi ya Dar es Salaam kama sehemu ya jitihada zake endelevu za Uwajibikaji wa Mamlaka kwa Jamii (CSR). Mpango huu unalenga kusaidia elimu na kuwawezesha wanafunzi kwa kuwapatia nyenzo muhimu za mafanikio. TMDA inaendelea kujitolea kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuchangia katika kukuza viongozi wa baadaye.*



*Dkt. Danstan Shewiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Maabara, akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu, alizindua rasmi Kamati ya Kiufundi ya Ufuatiliaji wa Usalama wa bidhaa za dawa tarehe 4 Machi 2025 mjini Morogoro. Tukio hili lilihusisha uteuzi wa wajumbe wapya wa kamati hiyo.*



*Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo (wa pili kushoto) akiwa pamoja na wanufaika wengine wa programu ya Shahada ya Uzamivu ya Mradi wa PROFORMA, wakati wa kongamano la kufunga mradi huo lililofanyika tarehe 18-19 Desemba nchini Uswidi.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, alitembelea Kiwanda cha Alfa Pharmaceuticals jijini Dar es Salaam tarehe 25 Machi 2025 kwa ajili ya kushughulikia changamoto za usajili wa dawa na kutoa mwongozo wa kitaalamu. Aliambatana na Dkt. Yonah Mwalwisi, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa, pamoja na Bw. Adonis Bitegeko, Meneja wa Kanda ya Mashariki wa TMDA.*




*Bodi ya Ushauri ya Waziri (MAB) katika mojawapo ya mikutano yake ya kawaida ya kusimamia shughuli za Mamlaka, iliyofanyika tarehe 20 Februari 2025 jijini Arusha.*




*Tarehe 18 Februari 2025, Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mb), alikutana na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Waziri (MAB) kwa TMDA jijini Arusha. Mazungumzo yao yalijikita katika kuimarisha udhibiti wa dawa nchini Tanzania ili kuboresha upatikanaji wa dawa nafuu. MAB ilikutana kwa kikao chake cha kawaida ili kupitia utendaji wa TMDA katika kulinda na kuendeleza afya ya umma.*

# Machapisho Zaidi ya Wanasayansi wa TMDA

*Katika kuonesha umahiri wa kisayansi na ubunifu, watafiti na wanasayansi wa TMDA kwa mara nyingine tena wamechangia kwa kiasi kikubwa katika maarifa ya kisayansi duniani kupitia mfululizo wa machapisho ya kisayansi yaliyopitiwa na wataalamu.*

*Machapisho haya hayadhihirishi tu dhamira ya TMDA katika kulinda afya ya jamii, bali pia yanaonesha uwezo wake wa kudhibiti bidhaa za dawa na shughuli za utafiti.*

*Machapisho haya yanayohusu mada mbalimbali ikiwemo ufuatiliaji wa usalama wa dawa baada ya kuingia sokoni, usalama wa dawa, usimamizi wa majaribio ya dawa, ufanisi wa dawa, na matumizi sahihi ya dawa, yanaakisi juhudi za muda mrefu za TMDA katika kuhakikisha ubora, usalama, na ufanisi wa bidhaa za afya zinazotumika nchini.*

*Baadhi ya machapisho ya hivi karibuni yaliyofanywa na wanasayansi wa TMDA na kuchapishwa kwenye majarida ya kisayansi ni pamoja na:*

- *Fimbo AM, Sillo HB, Nkayamba A, Kisoma S, Mwalwisi YH, Idris R, Asiimwe S, Githendu P, Ogbuoji O, Morrison L, Bump JB, Kaale E. Strengthening regulation for medical products in Tanzania: An assessment of regulatory capacity development, 1978–2020. PLOS Glob Public Health, 2024.*

- *Mwamwitwa KW, Bukundi EM, Maganda BA, Munishi C, Fimbo AM, Buma D, Muro EP, Sabiiti W, et al. Adverse Drug Reactions Resulting from the Use of Chiral Medicines... INQUIRY, 2024.*

- *Eulambius M. Mlugu et al. A Comparative Assessment of Quality of Antimalarial Medicines in Mainland Tanzania..., Am. J. Trop. Med. Hyg., 2024.*

- *Fimbo, A., Mwalwisi, Y.H., Matiko, D. et al. Lessons from enriching Tanzania's clinical research ethics... Discov Public Health, 2024.*

- *Sangeda RZ, Ndabatinya CJ, et al. Good manufacturing practice inspections... J Pharm Policy Pract, 2024.*


- *Fimbo AM, Mnkugwe RH, et al. Efficacy of ivermectin and albendazole combination... Infect Dis Poverty, 2024.*

- *Raphael Z Sangeda, et al. Antibiotic utilization patterns in Tanzania... JAC-Antimicrobial Resistance, 2024.*

*Machapisho haya, ambayo yanaweza kunukuliwa na kupatikana kupitia programu za utafutaji na vyanzo mbalimbali vya kitaalamu kama PubMed, Medline, Google Scholar, Elsevier, na Scopus, yanaonesha uwazi na uwajibikaji wa TMDA katika kushirikisha jamii kuhusu hatua zinazochukuliwa kufuatilia bidhaa za afya zinazosambaa nchini.*

*Aidha, machapisho haya yanatoa takwimu muhimu kwa watunga sera na wananchi ili kuelewa vyema kuhusu usalama, ufanisi, matumizi, na mwenendo wa matumizi ya dawa, ikiwemo matumizi mabaya.*

*Kupitia usambazaji wa taarifa hizi kwa jamii, TMDA inaendeleza ushirikiano wa kimataifa, kufanya maamuzi kwa kuzingatia Ushahidi wa kisayansi, na kukuza uwazi wa kisheria. Tafiti zaidi na bunifu bado zinaendelea, na mara zitakapokamilika, matokeo yake yatawekwa wazi kwa umma.*





# Mradi wa Proforma Wahitimishwa kwa Mafanikio Makubwa Katika Usimamizi Usalama wa Dawa Afrika Mashariki

*Mradi wa miaka mitano wa PROFORMA uliozinduliwa Aprili 2018 kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya usimamizi wa usalama wa dawa (pharmacovigilance) na ufuatiliaji baada ya dawa kuingia sokoni (post-marketing surveillance) katika ukanda wa Afrika Mashariki, umehitimishwa rasmi mwezi Desemba 2024.*

*Mradi huo ulifadhiliwa na Mfuko wa Ushirikiano wa Utafiti wa Majaribio ya Dawa kati ya Nchi za Ulaya na Zinazoendelea (EDCTP), kwa ruzuku ya jumla ya Euro milioni 3, ambapo Euro 240,696 zilitolewa kwa TMDA. Mradi huo umeleta mageuzi makubwa katika namna dawa na chanjo zinavyofuatiliwa usalama wake katika ukanda huu.*

*Kwa jina kamili, mradi huu uliitwa Pharmacovigilance Infrastructure and Post-Marketing Surveillance System Capacity Building for Regional Medicines Regulatory Harmonization in East Africa, na ulitekelezwa katika nchi za Tanzania, Ethiopia, Kenya, Rwanda na Sweden kupitia ushirikiano wa taasisi za kitaifa za udhibiti wa dawa, taasisi za elimu ya juu, vituo shirika vya WHO na Vituo vya Umahiri wa Kikanda (RCOREs).*

*Lengo kuu lilikuwa kujenga uwezo miongoni mwa wadhibiti, watoa huduma za afya, wanataaluma na wadau wengine katika kugundua, kutathmini na kuzuia madhara yanayohisiwa kusababishwa na dawa au chanjo.*

*Nchini Tanzania, utekelezaji ulifanywa na TMDA kwa kushirikiana kwa karibu na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).*

*Katika kipindi cha mradi, wataalamu 12 walipata mafunzo maalumu ya usimamizi wa usalama wa dawa na ufuatiliaji wa matukio baada ya matumizi ya dawa (cohort event monitoring).*

*Wataalamu hao walikuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha ufuatiliaji wa usalama wa tiba za kutumia dawa ya Dolutegravir kwa waathirika wa VVU na chanjo ya Janssen dhidi ya COVID-19.*

*Matokeo ya utafiti huo yalichapishwa katika majarida ya kisayansi na kuingizwa katika kanzidata ya kimataifa ya usalama wa dawa (Vigibase).*

*Mradi huu pia uliwezesha uzinduzi wa programu za uzamili katika fani ya pharmacovigilance katika vyuo vya MUHAS na Chuo Kikuu cha Addis Ababa, sambamba na kuimarisha programu iliyokuwepo katika Chuo Kikuu cha Nairobi.*

*Jumla ya wanafunzi 12 walidhaminiwa masomo kupitia mradi huu ambapo wanafunzi wanne wa Shahada ya Uzamivu (PhD) nchini Sweden na wanane wa Shahada ya Uzamili nchini Kenya na hivyo kuunda mtandao wa wataalamu watakaokuwa wawezeshaji na viongozi wa usimamizi wa dawa katika siku zijazo.*

*Matokeo ya mradi huu nchini Tanzania ni makubwa. Kabla ya PROFORMA, ripoti za madhara ya dawa kwa mwaka hazikuzidi 200. Tangu kuanza kwa mradi, idadi hiyo imeongezeka hadi zaidi ya 8,000 kwa mwaka.*

*Kati ya mwaka 2018 na Septemba 2024, zaidi ya matukio 62,000 yaliripotiwa kwenye hifadhidata ya kimataifa, hatua iliyoiweka Tanzania nafasi ya 47 kati ya nchi 168 kwa utoaji wa taarifa za usalama wa dawa duniani. Mafanikio haya yamechangiwa na mafunzo yaliyotolewa kwa zaidi ya wataalamu wa afya 9,000 nchini kote.*

*Aidha, PROFORMA ilisaidia kuanzisha na kuimarisha vituo vya kitaifa na vya kanda vya usimamizi wa usalama wa dawa kwa vifaa vya TEHAMA vinavyowezesha uingizaji wa data kwa wakati halisi.*

*TMDA pia iliandaa na kutekeleza kanuni mpya za usimamizi wa usalama wa dawa, ambazo zinalazimisha wadau kama watoa huduma, wamiliki wa vibali vya dawa (MAHs), na programu za afya ya umma kutoa taarifa za madhara ya dawa.*

*Hatua nyingine kubwa iliyofikiwa ni maandalizi ya Mpango Madhubuti yaa Usimamizi wa Usalama wa Dawa nchini, kufuatia tathmini ya awali kwa kutumia viashiria vya WHO.*

*Kutokana na juhudi hizo, Tanzania ilifikia Kiwango cha Umahiri wa Tatu (Maturity Level 3 - ML3) katika zoezi la tathmini ya WHO lililofanyika Julai 2024, ikiwa ni kiashiria cha mfumo madhubuti na endelevu wa kudhibiti usalama wa dawa na chanjo.*

*Pia, mmoja wa wafanyakazi wa TMDA aliyekamilisha masomo ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi alifanikiwa kupata ufadhili wa kufanya utafiti kuhusu usimamizi wa mnyororo baridi wa chanjo katika mkoa wa Arusha kupitia Kituo cha Umahiri cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Chanjo, Kinga na Usambazaji wa Huduma za Afya (EAC-RCE-VIHSCM).*

*Utafiti huo sasa umepanuliwa hadi Kaunti ya Nairobi nchini Kenya na Wilaya ya Bariadi nchini Tanzania, jambo linalooonesha mchango wa mradi katika kuchochea tafiti zenye tija kwa ukanda huu.*

*Wakati PROFORMA inavyohitimishwa, wadau wanatafakari mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha mifumo, ushirikiano wa kikanda na miundombinu ya mafunzo endelevu. "Mradi huu umeleta mapinduzi ya msingi katika namna tunavyoshughulikia usalama wa dawa Afrika Mashariki," alisema Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo.*

*"Umeimarisha mifumo yetu ya ufuatiliaji, umejenga uwezo wa wataalamu wetu na kuanzisha ushirikiano wa kitaaluma wa kudumu," Dkt. Fimbo alisema*

*Kwa sasa, mazingira ya udhibiti wa dawa katika kanda yameimarika na yako tayari kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa za afya.*

*Mradi wa PROFORMA umeweka msingi imara kwenye mfumo wa usimamizi wa usalama wa dawa, wenye ushirikiano na unaotegemea takwimu. Mfumo huu utanufaisha mamilioni ya watu Afrika Mashariki hata baada ya mradi kumalizika.*



# Vita ya Usugu wa vimelea dhidi ya dawa: Uhamasishaji kwenye ufugaji

*Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Antimicrobial Resistance - AMR) umeonekana kuwa ni tishio kubwa kwa afya duniani, unaoathiri binadamu, wanyama, na mazingira.*

*Nchini Tanzania, wasiwasi kuhusu usugu wa vimelea vya magojwa dhidi ya dawa unahusishwa kwa karibu na matumizi yasiyo sahihi na matumizi kupita kiasi ya dawa za kuua vimelea vya magonjwa (antimicrobials) si tu kwa binadamu bali pia kwa wanyama na kilimo.*

*Kwa kutambua uzito wa suala hili, TMDA imechukua hatua za makusudi za kupambana na ongezeko la usugu wa dawa, ikijikita zaidi katika uhamasishaji kwenye sekta ya Afya na ufugaji.*

*Usugu wa dawa hutokea pale viumbe hai kama vile bakteria, virusi, fangasi, na vimelea wanapobadilika na kuwa sugu kwa dawa zilizokusudiwa kuwaangamiza. Hii inafanya maambukizi kuwa magumu kutibu, kuongeza hatari ya kuenea kwa magonjwa, na kuongeza idadi ya vifo.*

*Katika ufugaji wa wanyama, matumizi mabaya ya dawa na kuzuia magonjwa bila uangalizi wa wtaalamu wa mifugo yamebainika kuwa chanzo kikubwa cha kuibuka kwa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa.*

*Kwa mujibu wa Bi Gaudensia Simwanza, Meneja wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa TMDA na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji kuhusu mapambano dhidi ya Vimelea (Awareness TWG) alisema: "Mamlaka imekuwa ikishiriki katika kupambana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa kupitia utekelezaji wa mpango mkakati, kampeni za uhamasishaji na elimu kwa umma na ushirikiano kati ya sekta mbalimbali za Serikali na washirika wa Maendeleo."*

*Bi Simwanza alieleza kuwa – "Kama sehemu ya juhudi za udhibiti wa Usugu wa vimelea dhidi ya dawa, TMDA inashiriki kikamilifu katika kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa (2023–2028), unaolenga kuwezesha matumizi bora ya dawa za kuua vimelea katika mazao ya mifugo na ufugaji wa wanyama."*

*Mchango muhimu wa Mamlaka ni usimamizi wake wa kisheria wa dawa za binadamu na za mifugo. TMDA inahakikisha kuwa ni dawa zilizojisajili na kuthibitishwa ubora pekee ndizo zinazopatikana katika soko na matumizi yake yanazingatia viwango vya kitaifa.*

*Mamlaka pia inasaidia programu za mafunzo kwa wataalamu wa mifugo, maafisa wa mifugo, na wakulima ili kuwasaidia kuelewa umuhimu wa matumizi sahihi ya dawa za kuua vimelea vya magonjwa na hatari zinazohusiana na kutotumia dawa kwa usahihi.*

*Uhamasishaji ni nyenzo kwa TMDA katika kupambana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa. Mamlaka inashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya, na wadau wengine katika kampeni za uelimishaji umma zinazohamasisha kinga na kudhibiti maambukizi katika ufugaji. Juhudi hizi zinakusudia kupunguza milipuko ya magonjwa na kupunguza utegemezi usio wa lazima kwa antibiotiki*

*TMDA pia inafanya ufuatiliaji wa kawaida na uchunguzi wa matumizi ya dawa za kuua vimelea na usugu. Kwa kusaidia maabara zinazoweza kufanya upimaji wa usugu wa dawa za kuua vimelea, Mamlaka inawawezesha madaktari wa mifugo na wataalamu wa afya ya wanyama kufanya maamuzi yanayotokana na ushahidi wanapopendekeza matumizi ya antibiotiki.*

*Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa ingawa asilimia 84 ya hospitali nchini Tanzania zinazingatia miongozo ya utoaji wa dawa,utoaji dawa za vijiuasumu (antibiotiki) nyingi likilinganishwa na matokeo ya maabara limejitokeza.*

*TMDA inashughulikia hili kwa kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya zana za uchunguzi katika dawa za binadamu na za mifugo. Juhudi za Mamlaka pia zinagusa ngazi ya msingi, ambapo inafanya kazi na wakulima ili kuwepo mbinu bora za ufugaji ikiwa ni pamoja na usafi bora, chanjo, na hatua za ulinzi ili kupunguza viwango vya maambukizi na haja ya matumizi ya antibiotiki.*

*Kwa kuwa kinga na kudhibiti maambukizi kunakuwa muhimu zaidi katika kuzuia AMR, jukumu la TMDA ni muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Kupitia udhibiti, elimu, na ushirikiano, TMDA inaendelea kujenga ustahimilivu wa kitaifa dhidi ya AMR, kulinda afya ya umma na uchumi wa mifugo.*

# Mfumo wa Uteketezaji wa Dawa zisizofaa waimarishwa

> **Tunatoa wito kwa vituo vyote vya afya, maduka ya dawa na wasambazaji kuzingatia kanuni bora za uhifadhi na uteketezaji wa dawa," alisisitiza Bw. Bitegeko. "Hili si suala la usimamizi wa taka pekee, bali ni suala la kulinda maisha ya watu na mazingira yetu."**

*Ofisi ya TMDA Kanda ya Mashariki imeongeza juhudi katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa ujumla kwa kuhakikisha uteketezaji sahihi wa dawa na vifaa tiba vilivyopitwa na muda, bandia au visivyofaa kwa matumizi ya binadamu.*

*Meneja wa TMDA Kanda ya Mashariki, Bw. Adonis Bitegeko, alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2024, Mamlaka ilifanikiwa kutekeza kwa usalama kiasi kikubwa cha dawa na vifaa tiba visivyofaa, hatua ambayo imesaidia kulinda afya ya jamii.*

*Kwa mujibu wa Bw. Bitegeko, wateja waliwasilisha dawa zilizopitwa na muda na zisizofaa zenye jumla ya uzito wa kilo 264,399.05 zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.88. Katika kipindi hicho hicho, vifaa tiba vyenye uzito wa kilo 38,533.61 viliteketezwa, vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 12.17. Bidhaa zilizokamatwa wakati wa ukaguzi wa kawaida pia ziliteketezwa, ikiwemo dawa zenye uzito wa kilo 7,120 na thamani ya shilingi milioni 299.27, pamoja na vifaa tiba vya kilo 6,390 vyenye thamani ya shilingi milioni 256.35.*

*Hata hivyo, alifafanua kuwa si bidhaa zote zilizokamatwa ziliteketezwa. Baadhi ya dawa na vifaa tiba vilivyokuwa bado vinafaa kwa matumizi, zenye thamani ya shilingi milioni 12.58 (dawa) na shilingi milioni 9.13 (vifaa tiba), viligawiwa upya kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kusaidia utoaji huduma za afya.*

*Zoezi la uteketezaji lilifanyika kwa ushirikiano na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), mamlaka za afya za mikoa husika, na vyombo vya ulinzi na usalama. Uteketezaji huo ulizingatia taratibu madhubuti za usalama wa kimazingira, ikiwa ni pamoja na kutumia mitambo ya kisasa ya kuchoma kwa joto kali sana kama iliyothibitishwa na NEMC.*

*Bw. Bitegeko alisisitiza juu ya hatari ya kuteketeza dawa vibaya. "Kutupa dawa hovyo, kama vile kwenye mashamba wazi au kuzimwaga kwenye mifumo ya maji, kunaweza kuchangia kuongezeka kwa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (antimicrobial resistance) na kuchafua vyanzo vya maji. Hili ni tishio kubwa kwa afya ya binadamu na mazingira," alionya.*

*Dawa zilizoteketezwa zilihusisha aina mbalimbali za dawa zinazotumika mara kwa mara kama vile antibiotiki, dawa za maumivu, dawa za malaria, pamoja na vifaa tiba mbalimbali. Dawa na vifaa hivi vilikusanywa kutoka vituo vya afya, maduka ya dawa na wasambazaji katika maeneo mbalimbali ya Kanda ya Mashariki.*

*TMDA inaendelea kuhimiza jamii, watoa huduma za afya, na wafanyabiashara wa dawa kuwasilisha dawa zilizopitwa na muda au zisizotumika katika ofisi za TMDA zilizo karibu badala ya kuzitupa kiholela.*

*"Tunatoa wito kwa vituo vyote vya afya, maduka ya dawa na wasambazaji kuzingatia kanuni bora za uhifadhi na uteketezaji wa dawa," alisisitiza Bw. Bitegeko. "Hili si suala la usimamizi wa taka pekee, bali ni suala la kulinda maisha ya watu na mazingira yetu."*

*Mchakato huu wa udhibiti unafuata viwango bora vya kitaifa na kimataifa katika usimamizi wa taka za dawa. TMDA imejidhatiti kuhakikisha kuwa taka za dawa zinadhibitiwa kwa njia salama na kwa kuzingatia misingi ya sheria, ili kulinda afya ya jamii na mazingira.*






# Wawekezaji Wahimizwa Kuwekeza Katika Sekta ya Dawa Tanzania

*Licha ya kwamba takriban asilimia 80 ya dawa zinazopatikana kwenye soko la Tanzania huagizwa kutoka nje, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jaffo, ameihimiza TMDA kushiriki kikamilifu na kuvutia wawekezaji katika sekta ya uzalishaji wa dawa na vifaa tiba ndani ya nchi.*

*Dkt. Jaffo alitoa wito huo tarehe 10 Septemba, 2024, alipotembelea banda la TMDA katika Maonesho ya 19 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza. Maonesho haya yalileta pamoja washiriki na wadau kutoka kanda nzima ya Afrika Mashariki.*

*"Tanzania kwa sasa inategemea sana dawa na vifaa tiba vinavyoagizwa kutoka nje, hali inayotoa fursa kubwa kwa uwekezaji katika uzalishaji wa ndani," alisema Dkt. Jaffo. "TMDA inafanya kazi ya kupongezwa katika kulinda ubora na usalama wa bidhaa za dawa. Huu ndio wakati sahihi kwa Mamlaka kuwashawishi wawekezaji wa nje kuanzisha viwanda vya dawa hapa nchini. Serikali tayari imeweka mazingira rafiki kwa uwekezaji na itaendelea kuboresha zaidi mazingira hayo."*

*Akitoa taarifa kwa Waziri, Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki, Bi. Sophia Mziray, alieleza dhamira ya Mamlaka ya kuwezesha biashara kupitia utoaji wa huduma za udhibiti kwa ufanisi na weledi.*

*"Tunaendesha shughuli zetu kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Wateja unaolenga utoaji wa huduma kwa wakati," alisema Bi. Mziray. "Aidha, TMDA imeweka wakaguzi katika bandari zote za kuingilia bidhaa ili kurahisisha uingizaji na usafirishaji wa bidhaa zinazodhibitiwa nchini."*

*Juhudi za TMDA zilitambuliwa rasmi kwenye maonesho hayo baada ya Mamlaka kutunukiwa tuzo ya mshindi wa kwanza katika kundi la taasisi za udhibiti kwa utoaji bora wa huduma.*

# Zaidi ya Asilimia 75 ya Wateja Wanaridhika na Huduma za TMDA

*Katika jitihada zake za kulinda afya ya jamii na kuboresha viwango vya utoaji huduma, TMDA imefanikiwa kukamilisha kwa ufanisi utafiti wake wa Tano (5) wa kiwango cha wateja kuridhika na huduma za Mamlaka (Service Delivery Survey - SDS) uliofanyika kati ya Novemba na Desemba 2024.*

*Utafiti huu uliofanyika nchi nzima unathibitisha dhamira ya TMDA katika kuboresha utoaji huduma kwa kuzingatia maoni ya wadau na wateja wake. Utafiti huu ulifanywa kwa ushirikiano kati ya wataalamu kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS) ambapo ulijumuisha taarifa muhimu kutoka wilaya 35 katika mikoa 16, ukihusisha makundi mbalimbali ya wadau ikiwa ni Pamoja na wafanyakazi wa TMDA, watengenezaji, waagizaji, wauzaji rejareja, watumiaji wa huduma za maabara, vyombo vya habari, na umma kwa ujumla.*

*Utafiti wa mwaka 2024, ambao ni wa kwanza tangu kubadilishwa kwa muundo wa TMDA mwaka 2019, ulijikita katika kupima kiwango cha wateja na wadau kuridhika na huduma zake, uelewa wa jamii kuhusu shughuli za udhibiti na utekelezaji wa viwango vya utoaji huduma za TMDA kama zilivyoainishwa katika mkataba wa huduma kwa wateja.*

*Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa wadau kwa ujumla wanaridhika na utendaji kazi wa TMDA, ambapo kiwango cha kuridhika kwa wateja wa nje ni asilimia 74.8 na kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi wa ndani ni kizuri ambacho ni asilimia 89.2. Hata hivyo, changamoto ya kuridhika kidogo kwa wafanyakazi na malipo (47.98%) na nyongeza za mishahara (40.81%) zimebainishwa, na hivyo kuhitaji mapitio na mageuzi ya kimfumo. Aidha, utafiti ulibaini ongezeko la kampeni za elimu kwa umma kuhusu shughuli za TMDA, kutoka asilimia 47 mwaka 2020 hadi asilimia 56 mwaka 2024, pamoja na uelewa wa wastani kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Wateja.*

*Licha ya mafanikio katika jukumu lake la udhibiti wa bidhaa, hasa katika kupunguza dawa bandia sokoni, utafiti bado umeonesha upungufu wa rasilimali kama kikwazo cha kupanua huduma ili kufikia maeneo ya pembezoni. Pia, mfumo wa utoaji huduma umebainika kuwa na mapungufu yanayohitaji kuwekewa mikakati ili kuboresha mikakati ya kutangaza huduma.*




*Ili kushughulikia mapengomapungufu hayo, utafiti umeainisha mapendekezo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha kampeni za elimu kwa umma, kufanya mapitio ya muundo wa mishahara, maboresho ya mifumo ya kieletroniki kwa ajili ya utoaji huduma za kidijitali, na kuimarisha ushirikiano na wadau.*

*Pia imependekeza hatua za haraka kama vile kuboresha mwonekano wa tovuti ya TMDA kwa ajili ya kupokea maoni na kushughulikia malalamiko, kuboresha kanzi data ya wateja, kuimarisha uhamasishaji wa huduma za maabara, na kuanzisha matukio ya kitaifa kama vile Wiki ya TMDA au mashindano ya michezo ili kuongeza uhusiano na ushirikiano wa umma.*

*Zaidi ya hayo, utafiti huu (SDS 2024) umedhihirisha dhamira ya TMDA katika uwazi, uwajibikaji, na utoaji huduma bora zinazozingatia mahitaji ya wateja. Kwa kusikiliza hoja za wadau na kujibu kwa wakati, TMDA inaendelea kujenga imani kwa jamii na kuimarisha jukumu lake kama taasisi ya udhibiti na usimamizi wa afya ya jamii.*

*Tafiti kuhusu kiwango cha wateja kuridhika na huduma hufanyika kila baada ya miaka minne ili kuchunguza kiwango cha kuridhika kwa wateja na wadau wengine na huduma zinazotolewa, kubaini kiwango cha uelewa na utekelezaji wa viwango vya utoaji huduma vilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TMDA. Pia hufka ili kubaini maeneo ya kuboresha ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa wateja na wadau wengine. Tafiti za awali wa zifanyika mwaka 2004, 2008, 2014, na 2020.*

# TMDA Yatoa msaada wa Dawa kwa Vituo vya Afya, Magereza katika mikoa ya Morogoro, Rukwa

*Kama sehemu ya mkakati wake ya kusaidia jamii (CSR), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) imetoa msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi milioni 38 kwa vituo vya afya na magereza katika mikoa ya Morogoro na Rukwa.*

*Mchango huu unalenga kuimarisha utoaji wa huduma za afya na kusaidia jamii zisizo na uwezo wa kupata huduma kwa urahisi, ikiashiria dhamira ya dhati ya TMDA katika kuboresha afya na ustawi wa wananchi kote nchini.*

*Katika Mkoa wa Morogoro, TMDA kupitia Ofisi yake ya Kanda ya Kati, ilikabidhi msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 19 kwa vituo vya afya vya magereza katika mkoa huo.*

*Msaada huu unatarajiwa kuboresha utoaji wa huduma katika vituo 13 vya afya vilivyopo katika magereza kwa kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu na kuimarisha afya katika magereza hayo.*

*Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Meneja wa TMDA Kanda ya Kati Bi. Sonia Henry Mkumbwa alisisitiza kuwa dawa na vifaa vilivyotolewa ni salama na vyenye ubora wa juu.*

*Alieleza kuwa kukabidhi msaada huu kunatokana na dhamira ya TMDA ya kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za dawa zilizothibitishwa ubora na usalama kwa Watanzania wote.*

*"Dawa hizi zilipatikana wakati wa ukaguzi na utekelezaji wa sheria uliofanyika Dodoma, Iringa, Singida, na Morogoro. Bidhaa hizi zilichukuliwa kutoka kwenye vituo ambavyo havikuwa na leseni ya kuhifadhi au kusambaza dawa hizo, kulingana na Kanuni za TMDA," alifafanua.*

*Akipokea msaada huo kwa niaba ya Kamishna Msaidizi wa Magereza (ACP) wa Kituo cha Magereza cha Morogoro, Bwana Godfrey Boniface Kavishe, ambaye ni Afisa Mkuu wa Magereza wa Mkoa, aliishukuru TMDA kwa hatua hizi za makusudi za kusaidia jamii.*

*"Dawa hizi zitaboresha huduma za afya katika vituo vyetu. Tumejizatiti kuzitumia kwa usahihi na kwa kufuata miongozo ya matibabu ya kitaifa," alisema.*

*Kwa upande mwingine, Ofisi ya TMDA ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilikabidhi dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 19 kwa Kituo cha Afya cha Tinda House kilichopo Mkoa wa Rukwa. Kituo hiki, kinachohudumia jamii ya vijijini isiyo na uwezo wa kupata huduma bora kinatarajiwa kunufaika na msaada huu.*

*Jitihada zote hizi ni sehemu ya mkakati wa TMDA wa kusaidia wahitaji ikiwemo makundi yaliyosahaulika na wale wanaoishi katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi.*

*Kwa kugawa dawa salama, bora na zenye ufanisi zilizopatikana kutoka kwa wauzaji wasiofuata sheria, TMDA inasaidia kupunguza ombwe la upatikanaji wa huduma za afya huku ikihakikisha viwango vya udhibiti vinazingatiwa.*

*TMDA inaendelea kuhakikisha kuwa bidhaa zote za dawa zilizopo hapa nchini Tanzania zinakidhi viwango vya ubora, usalama, na ufanisi. Mamlaka inaendelea kushirikiana na wadau kote nchini ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kuchangia katika kuboresha huduma za afya nchini.*






# Ofisi ya TMDA Kanda ya Kusini Yahamia Ruvuma

*Kama sehemu ya jitihada zake endelevu za kuboresha utoaji wa huduma na kusogeza huduma za udhibiti karibu zaidi na wananchi, mwezi Septemba 2024, TMDA ilihamisha rasmi Ofisi yake ya Kanda ya Kusini kutoka Jengo la PSSSF, Mtwara hadi kufika Songea, Mkoa wa Ruvuma.*

*Uamuzi huu wa kimkakati unalenga kupunguza gharama za uendeshaji na kupunguza usumbufu kwa wateja, huku ukihakikisha mazingira rafiki na yenye ufanisi zaidi kwa utoaji wa huduma..*

*Maboresho haya yataiwezesha Mamlaka kuendelea kutekeleza dhamira yake ya kulinda afya ya jamii kupitia usimamizi madhubuti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.*

*Ofisi ya Kanda ya Kusini inahudumia wateja kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma, na inaendelea kutoa huduma bora za udhibiti kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.*

*Anuani Mpya ya Mawasiliano:*
*Ofisi ya TMDA – Kanda ya Kusini*
*Jengo la NBC, Ghorofa ya Kwanza*
*S. L. P. 48*
*Barabara ya Serengeti*
*Songea – Ruvuma*
*Simu: +255 766 729 416*
*Toll-Free: 0800 110084*
*Barua pepe: info.ruvuma@tmda.go.tz*

*TMDA inawakaribisha wadau na wateja wote wa Kanda ya Kusini kufika ofisi hii mpya kwa ajili ya kuendelea kupata huduma na msaada wa karibu.*




# TMDA Yang'ara SHIMMUTA 2024 Mchezo wa Netiboli

> *kizungumza wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo, mratibu wa michezo, Bw. Japhari Mtoro, alisema anajivunia umahiri na jitihada za timu: "Ufanisi huu hauonyeshi tu umahiri wa kimichezo bali pia umoja, nidhamu, na juhudi zinazotutambulisha kama taasisi. Tunashukuru Uongozi kwa msaada na wafanyakazi wote kwa maombi yao."*

*Katika dhana ya mshikamano na kuonesha vipaji, TMDA inajivunia kushika nafasi ya pili katika mchezo wa netiboli kwenye mashindano ya SHIMMUTA 2024, yaliyofanyika kuanzia tarehe 10 hadi 24 Novemba 2024 katika Jiji la Tanga.*

*Mashindano ya SHIMMUTA (Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi, na Makampuni Binafsi Tanzania) yalileta pamoja wafanyakazi kutoka taasisi mbalimbali za umma kote nchini kwa ajili ya kuimarisha mshikamano na umoja wa kitaifa. Timu ya TMDA, iliyojumuisha wanamichezo na wanariadha kutoka ofisi za kanda na makao makuu, ilishiriki kikamilifu katika mashindano haya.*

*Timu za TMDA, ikiwa ni pamoja na timu ya netiboli, mpira wa miguu, na riadha, zilionyesha nidhamu, weledi na ustadi katika michezo mbalimbali kipindi cha mashindano. Jitihada za wachezaji katika mazoezi na kujenga afya pamoja na mkazo wa taasisi katika michezo zimeleta mafanikio haya makubwa.*

*Akizungumza wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo, mratibu wa michezo, Bw. Japhari Mtoro, alisema anajivunia umahiri na jitihada za timu: "Ufanisi huu hauonyeshi tu umahiri wa kimichezo bali pia umoja, nidhamu, na juhudi zinazotutambulisha kama taasisi. Tunashukuru Uongozi kwa msaada na wafanyakazi wote kwa maombi yao."*

*Ushiriki wa TMDA katika mashindano ya SHIMMUTA unaonesha dhamira yake ya kuleta usawa kati ya utekelezaji wa majukumu ya udhibiti kwa ufanisi, utimamu wa afya ya mwili ya wafanyakazi na maendeleo ya jamii. Michezo hii inatoa nafasi kwa watumishi kuimarisha ushirikiano, kuleta ustawi, na kuongeza morali huku ikisisitiza umuhimu wa kulinda afya na ushirikiano katika maendeleo ya kitaifa.*

*TMDA inapojipanga kwa ajili ya mashindano ya mwaka ujao, mafanikio ya 2024 katika Jiji la Tanga yanabaki kuwa alama ya ushindi, uoneshaji wa vipaji, ustahimilivu, na umahiri katika.*

*Hongera, TMDA!*

# TMDA Yakabidhi Maabara Hamishika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu

*Katika juhudi za kuimarisha afya ya jamii na kuhakikisha upatikanaji wa dawa salama, bora na zenye ufanisi, TMDA ilikabidhi Maabara Hamishika moja kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu tarehe 11 Novemba 2024.*

*Akizungumza katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika mkoani Simiyu, Meneja wa Ofisi ya TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki, Bi. Sophia Mziray, alisisitiza umuhimu wa kifaa hicho katika kubaini dawa zisizokidhi viwango kabla hazijaanza kutumika na wananchi.*

*"Maabara Hamishika hii huwezesha uchunguzi wa haraka na wa gharama nafuu wa ubora wa dawa, pia imeundwa kwa namna inayoiwezesha kufanya uchunguzi wa sampuli nyingi kwa wakati mmoja ndani ya muda mfupi," alieleza Bi. Mziray.*

*Aliongeza kuwa kifaa hiki kitaongeza uwezo wa kulinda afya ya jamii kwa kubaini kwa wakati dawa hafifu, na kuiwezesha TMDA kuchukua hatua stahiki kwa haraka.*

*Akizungumza kwa niaba ya mkoa wa Simiyu wakati wa kupokea kifaa hicho, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Kenan Kihongosi, aliishukuru TMDA kwa juhudi zake katika kulinda afya ya jamii.*

*"Tunashukuru kwa msaada huu wa kipekee. Tayari tumetenga eneo maalum katika hospitali kwa ajili ya kifaa hiki, na wataalam wetu wa afya wamepewa mafunzo ya kukitumia. Hakika hii ni hatua kubwa ya kuboresha usalama na ubora wa dawa katika mkoa wa Simiyu na maeneo jirani," alisema.*

*Aidha, alitoa rai kwa uongozi wa hospitali kuhakikisha kifaa kinatunzwa ipasavyo, akisisitiza kwamba, "Hiki si kifaa cha kawaida; ni chombo cha kuokoa maisha. Matumizi sahihi ya kifaa hiki yatachangia moja kwa moja katika kuboresha afya ya wananchi wetu."*


*Maabara Hamishika imelenga kufanya uchunguzi wa awali wa dawa zinazotumika katika matibabu ya magonjwa yanayofuatiliwa kwa karibu kama vile malaria, UKIMWI, kifua kikuu, minyoo ya tumbo, na maambukizi ya bakteria.*

*TMDA ilianzisha matumizi ya Maabara Hamishika kwa mara ya kwanza mwaka 2002 ikiwa na mashine tano pekee. Hadi sasa, jumla ya maabara hamishika 26 zimepatikana na kusambazwa kwa matumizi katika hospitali za rufaa za mikoa pamoja na vituo vya forodha, hatua inayosaidia kuongeza uwezo wa taasisi kufanya uchunguzi wa haraka wa ubora wa bidhaa za afya.*



# TMDA Yawaaga Watumishi Wake Waliotumikia kwa Muda Mrefu

*Kwa heshima na shukrani za dhati, TMDA hivi karibuni iliwaaga rasmi watumishi wake watatu waliotumikia taifa kwa muda mrefu kwa uadilifu na moyo wa kujituma ambao ni Bw. Oscar Kandege, Bw. Oscar Mbafu, na Bw. Hamad Lyimo kufuatia kustaafu rasmi utumishi wa umma.*



**Bw. Oscar Kandege**

*Bw. Oscar Kandege alikuwa miongoni mwa waanzilishi waliotoka Bodi ya Famasi ya zamani hadi kuanzishwa kwa TFDA mwaka 2003. Alilitumikia taifa kwa moyo wa kutumika katika Kurugenzi ya Huduma za Maabara akiwa fundi wa vifaa vya maabara. Alikuwa nguzo muhimu katika uanzishwaji na uendeshaji wa maabara ya Udhibiti Ubora ya TMDA, akitoa mchango mkubwa katika kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vipimo nchini.*

*Katika kipindi chote cha utumishi wake, Bw. Kandege alionyesha ufanisi mkubwa katika ufungaji, upimaji na matengenezo ya vifaa vya maabara, na mchango wake mkubwa ulihakikisha bidhaa zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.*

*Aliacha alama isiyofutika kupitia ripoti nyingi za uchambuzi na mapendekezo ya udhibiti aliyoyasimamia, pamoja na kukuza utamaduni wa nidhamu na ubora ndani ya maabara za TMDA. Akiwa Katibu wa TUGHE kati ya mwaka 2005 hadi 2020, alitoa mchango mkubwa katika kuwatetea na kuwahudumia wafanyakazi.*

*Anapoingia katika maisha ya kustaafu, Bw. Kandege anaacha alama madhubitu ya utumishi wake katika maabara pamoja na timu ya wataalamu wanaoendeleza viwango alivyovisimamia kwa miaka mingi.*

# TMDA Yawaaga Watumishi Wake Waliotumikia kwa Muda Mrefu



**Bw. Oscar Mbafu**

*Bw. Oscar Mbafu alilitumikia Shirika kwa moyo wa kujituma tangu mwaka 2017, enzi za TFDA, akifanya kazi kama dereva katika ofisi mbalimbali za TMDA, ikiwemo Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa Mashariki. Katika utumishi wake, alijulikana kwa weledi, uaminifu, na bidii ya kazi.*

*Mbali na kusafirisha watumishi na nyaraka, Bw. Mbafu alikuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa maeneo, mikutano ya wadau, na kampeni za elimu kwa umma, hasa katika maeneo ya pembezoni. Ujuzi wake mkubwa wa barabara na maeneo ya nchi ulikuwa msaada mkubwa kwa Mamlaka.*

*Alikuwa maarufu miongoni mwa wenzake kwa unyenyekevu, nidhamu na moyo wa ushirikiano. Alijulikana kwa kuwa mtulivu, mwenye heshima, na mtu wa kujitolea kufanya kazi zaidi ya wajibu wake.*

*Ingawa mchango wake ulikuwa nyuma ya pazia, huduma ya Bw. Mbafu ilikuwa muhimu katika kufanikisha jukumu la TMDA la kulinda afya ya jamii. Mamlaka inatoa shukrani za dhati kwa uaminifu, kujitoa na utendaji wake uliotukuka.*



**Bw. Hamad Lyimo**

*Bw. Hamad Lyimo alijiunga na TMDA mwaka 2022 akitokea TAMISEMI akiwa na uzoefu mkubwa wa huduma za usafiri wa viongozi. Akiwa Dereva Mkuu, alihudumu kwa umahiri katika ofisi ya TMDA Kanda ya Kati, Dodoma, ambako alijijengea heshima kutokana na uwezo wake wa kuendesha kwa usalama, nidhamu na uwajibikaji.*

*Alihakikisha usafiri salama na kwa wakati wa watumishi na nyaraka muhimu katika mikoa ya kanda hiyo. Uelewa wake mzuri wa uratibu wa shughuli za usafirishaji na kanuni za usalama barabarani ulimfanya kuwa tegemeo muhimu katika kazi mbalimbali za TMDA, zikiwemo ziara za wadau na kazi za ukaguzi wa maeneo.*

*Zaidi ya ujuzi wake wa kuendesha, Bw. Lyimo aliheshimika kwa unyenyekevu, kuwahi kazini na kusaidia wafanyakazi wa ngazi mbalimbali kwa moyo wa ushirikiano. Mchango wake uliimarisha taswira chanya ya TMDA katika Kanda ya Kati.*

## *Hitimisho*

*TMDA inatoa pongezi za dhati kwa Bw. Kandege, Bw. Mbafu, na Bw. Lyimo kwa huduma yao ya mfano, uadilifu, na mchango wao mkubwa katika kutimiza dhamira ya Mamlaka ya kulinda afya ya umma. Uzoefu, kumbukumbu za taasisi na ari yao ya kazi vitabaki kuwa sehemu ya urithi wao wa kudumu.*

*Wanapoanza ukurasa mpya wa maisha ya kustaafu, Mamlaka inawatakia heri na baraka tele wao na familia zao, na kuwatambua kuwa mchango wao bado unathaminiwa na unahitajika.*

*Hakika wanaondoka kazini lakini alama zao za utumishi zinabakia.*

# Furaha ya ushindi wa mpira wa Pete katika Mashindano ya SHIMMUTA








# Michezo huimarisha utendaji kazi wetu mahali pa kazi









# Michezo huimarisha utendaji kazi wetu mahali pa kazi









P.O. Box 1253, Dodoma or P.O. Box 77150, Dar es Salaam, Tanzania.
**Telephone:** +255 22 2450512 / 2450751 / 2452108
**Fax:** +255 22 2450793
**Email Address**: info@tmda.go.tz